The Guardian Uk.6, Tarehe 18/12/2020

# Musoma fishermen directed to form groups to access loans from banks

**By Guardian Correspondent, Musoma**

FISHERMEN in Busekera, Bwai, Kumsoma shores and in Lake Victoria islands of Iriga and Bukuba in Mara Region have been called on to form groups in order to access loans from Musoma District Council and other financial institutions.

Likewise, they have been urged to abide by laws, regulations and other procedures governing harvests of lake resources.

The call was given on Wednesday this week by Musoma District Fisheries Officer, Augustine Constantine during the visit by the district's officials to the fishermen aimed at improving fishing activities.

The entourage included the District Community Development Officer, Tanna Nyabange, his assistant Nyanjara Majura and officials from Equity Bank who mobilised fishermen to open accounts with the bank.

Nyabange said it was important for fishermen to transform the sub sector by abiding by laws, regulations and other procedures on fishing, and abandon the use of illegal fishing gear and that every fisherman should be a guardian and teacher of fellow fishermen.

He said the District Council will continue providing training to fishermen so that all fishing areas become safe and called on them not to contravene any laws.

Tanna Nyabange, the district's community development officer called on the fishermen to form groups in order to access loans from Musoma District Council and other financial institutions.

For their part, Equity Bank officials mobilised the fishermen to open accounts with the bank to access loans to strengthen their fishing activities.

Kemilembe Kabugumila, an Equity Bank official said they have registered 79 fishermen groups with 1,035 members which the bank will begin with in providing loans.

"We Equity Bank officials will first meet with the Musoma District Commissioner Dr Vincent Anney and the Constituency's Member of Parliament Prof Sospeter Muhongo to discuss loans opportunities to fishermen groups in Musoma rural areas," said Kabugumila.

He said the bank was ready to dish out loans to the fishermen's groups and the arrangements were underway, including discussion with the DC and the MP to make the exercise a success.


Get Free

| Free E-Paper for One Month | | Free Social Media Post | |
|---|---|---|---|
| The Guardian | Nipashe | Guardian or Nipashe | Guardian or Nipashe |


Scanned with CamScanner

UHURU

MAONI YA MHARIRI

# Operesheni kufunga bucha za nyama zisizozingatia masharti iwe ya kudumu

BODI ya Nyama Tanzania, imeanza rasmi operesheni ya kufunga mabucha yasiyozingatia masharti ya uuzaji wa bidhaa hiyo katika Jiji la Dar es Salaam.

Kaimu Msajili wa Bodi ya Nyama, Imani Sichwale, aliiambia Uhuru, juzi, kuwa operesheni hiyo inahusisha ukaguzi wa mabucha yote yasiyozingatia masharti ya uuzaji wa nyama.

Pia, alisema operesheni hiyo itayahusu mabucha yasiyozingatia usafi, matumizi ya nondo zenye kutu, badala ya aluminium na kusababisha nyama kutokuwa salama kwa matumizi ya walaji.

Kwa mujibu wa Sichwale, bucha zitakazobainika kuwa na mazingira ya uchafu, zinazotumia magogo na nondo chafu zenye kutu, zitafungiwa iwapo hazitarekebishwa, ikiwa ni pamoja na wamiliki kutozwa faini ya sh. 100,000.

Amesisitiza kuwa operesheni hiyo ni endelevu na imeanza Dar es Salaam, katika wilaya za Temeke, Ilala na baadaye itahamia Kinondoni.

Tunaipongeza Bodi ya Nyama kwa uamuzi wake huo, ikizingatiwa kuwa mabucha ni miongoni mwa maeneo nyeti ya kibiashara, hivyo yanapaswa kufuata taratibu za uendeshaji ili kulinda afya za walaji.

Ieleweke kuwa nyama ni miongoni mwa mboga zinazotumiwa na watu wengi, wakiwemo wafanyabiashara wanaomiliki hoteli zinazouza vyakula na pia kinamama na baba ntilie wanaoendesha biashara za vyakula, hivyo ni muhimu muda wote bidhaa hiyo ipatikane ikiwa katika ubora unaotakiwa.

Aidha, mabucha ya nyama yametapakaa katika maeneo mengi ya Jiji la Dar es Salaam, mengine yakiwa kwenye vichochoro vya mitaa na maeneo yanamopita maji machafu ama kulikorundikwa uchafu wa kila aina, hivyo usafi ni muhimu kwa wauzaji.

Hivyo ni vyema wamiliki wote wa bucha za nyama, kuendesha biashara hiyo katika mazingira safi na salama, ikiwa ni pamoja na kuzingatia masharti ya uuzwaji ili kuongeza soko la bidhaa hiyo hapa nchini.

Ni vyema pia wauzaji wa nyama wakawatumia wataalamu wa bidhaa hiyo, kabla ya kuiingiza sokoni kwa kuwa ndio wenye uwezo wa kujua usalama wa mnyama kwa ajili ya matumizi ya binadamu. Hii itasaidia kuingiza sokoni nyama ikiwa salama kwa matumizi.

Tunasema hivyo kwa sababu zipo baadhi ya nyama zimekuwa zikiuzwa holela na imekuwa ikidaiwa kuwa, zinatokana na mifugo iliyokufa kutokana na magonjwa ya aina mbalimbali au ukosefu wa chakula na maji kutokana na kusafirishwa kwa muda mrefu.

Hivyo, badala ya ukaguzi huo kuishia kwenye bucha za nyama pekee, ni vyema ukafanyika na kwenye maeneo, ambako bidhaa hiyo inauzwa holela, tena kwa mafungu, kwa lengo la kudhibiti ubora.

Pengine litakuwa jambo la muhimu zaidi iwapo kwa Bodi ya Nyama, itaamua kupiga marufuku kabisa uuzaji wa nyama holela, hasa zile zinazouzwa kwa mafungu kwa sababu inaonekana wazi kuwa hata upatikanaji wake ni wa mashaka.

Tunatoa wito kwa Bodi ya Nyama, kuifanya operesheni hii iwe ya kudumu na pia kuendelea kutoa elimu kwa wauzaji kuhusu taratibu zote muhimu wanazopaswa kuzifuata ili kurekebisha dosari zinazojitokeza mara kwa mara.

Ajali>> Ilala inaongoza kwa ku

HOJA YA HAJA

**Ninakubalia hiyo kwani zinaonyesha mwaka 201 watu 2,160, maisha kut za bodabod**

# Ushauri wa Rais kuhusu bodabo

RAIS mstaafu, Dk. Jakaya Kikwete, hivi karibuni alisimulia miaka 10 ya machungu na mafanikio ya hatua aliyoichukua ya kurasimisha usafiri wa pikipiki, maarufu 'bodaboda'.

Pamoja na masuala mengine, Dk. Kikwete, alishauri mamlaka

**Pamoja na masuala mengine, Dk. Kikwete, alishauri mamlaka husika kuhakikisha zinaweka mkakati madhubuti wa viwango vya kofia ngumu wanazovaa waendesha pikipiki.**

husika kuhakikisha zinaweka mkakati madhubuti wa viwango vya kofia ngumu wanazovaa waendesha pikipiki.

Alishauri kofia zinazoingizwa na zile zinazotengenezwa hapa nchini, ziwe na ubora siyo kama ilivyo sasa, ambapo kuna kofia, ambazo hata ukipiga konzi, zinatoboka.

Aliyasema hayo alipokuwa akikabidhi kofia ngumu 850, kwa bodaboda mkoani Dar es Salam, zilizotolewa na Taasisi ya Automobile Association Of Tanzania (AAT), kwa udhamini wa Taasisi ya Kimataifa ya Fia.

Alisema licha ya urasimishaji huo kuwa na mafa ikiwa ni pamoja changamoto y kurahisisha mais wamekuwa char katika familia nyi kusababisha ajali

Kikwete, a wa miaka 10 bodaboda kam usafiri nchini, mengi mabaya r

Lakini pia bodaboda, up pili, ambao s Bodaboda ni p cha simanzi kat zinazoondokew wao au wengi vilema vya kudu

Ninakubalia kwani takwim kuwa, kati ya m 2019, watu 2, maisha kutok bodaboda nchi

Nchi nzim 5,213, kati ya na asilimia 4 bodaboda, jar zuri na linas mengi kwenye

Takwimu Tiba ya Mifup zinaonyesha k na Desemba majeruhi 1 bodaboda w

TULIKOTOKA

Scanned with CamScanner

## ...kero ya maji

Alisema hadi kufikia sasa, DAWASA imeshalaza mabomba ya kilomita 2.3 ya nchi 6.4 hadi 8.

Mhandisi Fumbuka alisema hatua inayoendelea kwa sasa ni kuchimba mitaro.

# Wizara ya Mifugo yaja na mipango saba yenye tija

**Na Dotto Mwaibale, Singida**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imekuja na mipango saba yenye lengo la kuboresha tija ya uzalishaji wa mifugo hapa nchini.

Hayo yalielezwa na Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ugani, Dkt. Kejeri Gillah wakati wa kikao kazi cha washauri wa mifugo wa mikoa na wataalamu wa wizara katika kutekeleza mikakati ya sekta ya mifugo kuendana na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Singida juzi.

Alisema katika mwaka wa fedha 2018/19, wizara imeandaa na kuanza kutekeleza mikakati saba ili kuendeleza Sekta ya Mifugo nchini. Utekelezaji wa mikakati hiyo utaisaidia wizara kufikia dira na maono iliyojiwekea tangu awali kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Mifugo ya 2006.

Gillah alitaja malengo ya mikakati hiyo ni kuongeza uzalishaji na tija, kudhibiti utoroshaji na biashara haramu za mifugo na mazao yake, kudhibiti upotevu wa mapato yatokanayo na mifugo na mazao yake ili sekta iweze kuchangia kikamilifu kwenye pato la taifa, kuepusha migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, kulinda rasilimali za mifugo zilizopo na kuhifadhi mazingira.

Dkt. Gillah alitaja mikakati inayotekelezwa na wizara hiyo kuwa ni kuboresha kosaafu za ng'ombe nchini, kudhibiti magonjwa na matumizi ya dawa, chanjo na viuatilifu vya wanyama nchini, kutafutia ufumbuzi wa kudumu migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Alitaja mingine kuwa ni upatikanaji wa uhakika wa malisho na maji kwa mifugo, kuanzisha na kuwezesha ushirika wa wafugaji, kudhibiti upotevu wa mapato yatokanayo na biashara ya mifugo na mazao yake na kuboresha uzalishaji na biashara ya ndege wafugwao nchini.

Alisema tangu kuanza kwa utekelezaji wa mikakati hiyo katika maeneo mbalimbali nchini, wataalamu wa wizara wanaosimamia utekelezaji wa mikakati hiyo wamebaini uwepo wa elimu duni ya ufugaji bora na wa kibiashara kwa wafugaji walio wengi, hususan wenye mifugo mingi na wanaohamahama na mifugo yao.

Awali akifungua kikao kazi hicho Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Deogratius Yinza alisema sekta ya mifugo ni miongoni mwa sekta za kiuchumi ambayo ni muhimu katika kuondoa umaskini na kukuza uchumi wa taifa kwa ujumla.

Alisema Tanzania ina rasilimali ya mifugo ambayo wizara inasimamia na kwa sasa inakadiriwa kufika ng'ombe milioni 33.4, mbuzi milioni 21.29, kondoo milioni 5.65, kuku wa asili milioni 38.77, kuku wa kisasa milioni 44.51, nguruwe milioni 2.14 na punda wapatao 657,389.

Scanned with CamScanner